

NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Ridván 2024

Kwa Wabahá'í wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Miaka miwili ya jitihada za kuogofya za miaka tisa imepita kwa kasi. Marafiki wa Mungu wameyapokea malengo yake kwa uthabiti moyoni. Katika ulimwengu mzima wa Kibahá'í kuna kina kiongezekacho cha uelewa kuhusu kile kinachohitajika kuendeleza zaidi mchakato wa ujengaji jumuiya na kusababisha mabadiliko ya ndani kabisa ya kijamii. Lakini kwa kila siku ipitayo, tunaona vile vile hali ya ulimwengu ukiendelea kukata tamaa zaidi, migawanyiko yake mikubwa zaidi. Wasiwasi uongezekao ndani ya jamii na baina ya mataifa huathiri watu na maeneo kwa namna nyingi sana.

Hili huhitaji mwikio kutoka kwa kila roho yenye dhamira njema. Sote tunafahamu pia kwamba jumuiya ya Jina Kuu Kabisa haiwezi kutarajia kutoathiriwa na mateso ya jamii. Hata hivyo, ingawa huathiriwa na mateso haya, haikanganywi nayo; inahuzunishwa na shida za binadamu, lakini haivunjwi moyo nazo. Shauku ya dhati sharti ichochee juhudi endelevu za kujenga jumuiya ambazo hutoa matumaini badala ya kukatisha tamaa, umoja badala ya migogoro.

Shoghi Effendi alielezea kwa udhahiri jinsi mchakato wa “uharibifu uendeleo wa shughuli za kibinadamu” unavyotokea sanjari na mchakato mwingine, mchakato wa uunganishaji, ambao kupitia huo “Safina ya wokovu wa wanadamu”, “kimbilio la mwisho” la jamii, inaendelea kujengwa. Tunafurahia kuona, katika kila nchi na eneo, watendaji wa kweli wa amani wakijishughulisha na ujenzi wa kimbilio hili. Tunauona katika uwajibikaji wa kila moyo ukiwashwa kwa upendo wa Mungu, familia ikifungua nyumba yake kwa marafiki wapya, wenzi wakitumia mafundisho ya Baha'u'lláh kutatua matatizo ya kijamii, jumuiya ikiimarisha desturi ya kusaidiana, ujirani au kijiji vikijifunza kuanzisha na kudumisha matendo ya lazima kwa ajili ya maendeleo yake yenyewe ya kiroho na kimwili, eneo likibarikiwa kwa uibukaji wa Baraza jipya la Kiroho.

Mbinu na nyenzo za Mpango huiwezesha kila roho kuchangia sehemu ya kile ambacho binadamu huhitaji katika siku hii. Mbali na kutoa kitulizo cha muda kwa ajili ya matatizo ya wakati huu, utekelezaji wa Mpango ni mbinu ambayo kwayo mchakato ya ujengaji, ya muda mrefu, inayokunjuka kizazi hadi kizazi, inaanzishwa katika kila jamii. Haya yote hulenga kwenye hitimisho la haraka, lisiloepukika: Sharti pawepo na ongezeko endelevu la kasi la wale wanaotoa muda wao, nguvu zao, umakinifu wao kwenye mafanikio ya kazi hii.

Wapi kwingine bali katika kanuni ya Baha'u'lláh ya umoja wa jamii ya binadamu ambako ulimwengu unaweza kupata muono mpana vya kutosha kuunganisha vipengele vyake vyote anuwai? Kwa namna gani nyingine bali kwa kutafsiri muono huo katika utaratibu uegemeo juu ya umoja katika anuwai ambavyo ulimwengu unaweza kuponya mipasuko ya kijamii inayougawa? Nani mwingine awezaye kuwa chachu ambayo kwayo watu wa ulimwengu

wanaweza kugundua njia mpya ya maisha, ambayo ni njia ielekeayo amani ya kudumu? Basi nyoosheni kwa kila mtu mkono wa urafiki, wa jitihada ya pamoja, wa huduma ya pamoja, wa ujifunzaji wa pamoja, na songeni mbele kama kitu kimoja.

Tunatambua ni kiasi gani cha uchangamfu na nguvu kinachozalishwa katika jamii yoyote na vijana wake wanaoamshwa kuelekea muono wa Baha'u'lláh na kuwa manguli wa Mpango. Na hivyo, ni kwa wema mkubwa kiasi gani, ujasiri, na kumtegemea kabisa Mungu sharti vijana wa Kibahai waazimie kuwafikia vijana wa rika lao na kuwaleta katika kazi hii! Wote sharti wasonge mbele, lakini vijana sharti wapae.

Uharaka wa saa ya sasa haupaswi kuzuia furaha maalum ambayo hutokana na huduma. Mwito kwa huduma ni wito uinua, ukumbatio vyote. Huvutia kila roho aminifu, hata zile zielelewazo na majukumu na wajibu. Kwa kuwa katika njia zote ambamo roho hiyo aminifu inajishughulisha mnaweza kugundulika ibada iliyojikita mizizi na shauku ya milele kwa ajili ya usitawi wa wengine. Sifa kama hizo huleta upatano kwa maisha yenye mahitaji mengi. Na nyakati nzuri kabisa kati ya zote za moyo uliowashwa ni zile zilizotumiwa kuwa pamoja na kina dada na kina kaka wa kiroho, wakihudumia jamii yenye uhitaji wa kusitawishwa kiroho.

Katika Makaburi Matakatifu, kwa mioyo ifurikayo, tunamshukuru Baha'u'lláh kwa kuwainua na kuwafunza katika njia Zake, na tunamsihi Yeye awashushie baraka Zake.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu